TANGAZO LA SERIKALI NA 733 Tarehe 04/10/2019

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
SURA YA 287

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 153*

SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA NANYUMBU ZA MWAKA, 2019

## SEHEMU YA KWANZA:
## UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu za Mwaka, 2019.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Mtumishi yoyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Eneo la Hifadhi" maana yake ni maeneo ya milima, mbuga za wanyama, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi.

"Hifadhi ya Mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na Afisa Mwidhiniwa chini ya Sheria Ndogo hizi au Sheria nyingine yoyote.

"Kiwanda" maana yake ni jengo, majengo au eneo ambapo vitu vinatengenezwa au kuzalishwa kwa kutumia mashine au mitambo mikubwa au midogo.

"Kuvuna misitu" maana yake ni kufyeka, kukata au kung'oa miti, kwa njia endelevu baada ya kupata kibali kutoka Mamlaka husika.

"Maeneo ya malisho" maana yake ni sehemu zote ambazo zimetengwa na Halmashauri au Kijiji kuwa maeneo ya Malisho ya mifugo kupitia mpango wa matumizi bora ya ardhi.

"Maji" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira 2004.

"Maji taka" maana yake ni kama ilivyo tafsiriwa katika Sheria ya Mazingira 2004.

"Mazao ya misitu" maana yake kama ilivyo tafsiriwa katika Sheria ya Misitu Na.14 ya mwaka 2002 chini ya kifungu cha 2.

"Mazingira" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

"Mfugaji" maana yake ni mtu yeyote anayejishughulisha na ufugaji mifugo katika eneo la Halmashauri.

"Mifugo" maana yake ni mifugo yoyote inayofugwa na binadamu.

"Misitu" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 ya miti, uoto wa asili au iliyopandwa, au asilimia 50 au zaidi, ya vichaka na miti na miti inayoota upya ambayo itajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangazwa chini ya Sheria ya Misitu Na.14 ya mwaka 2002 na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri.

"Taka" maana yake ni kama ilivyo tafsiriwa katika Sheria ya Mazingira 2004.

"Taka Ngumu" maana yake ni kama ilivyo tafsiriwa katika Sheria ya Mazingira 2004.

"Taka za Viwandani" maana yake ni kama ilivyo tafsiriwa katika Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

"Uchafu Hatari" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika kifungu cha 133(5) cha Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

"Uchafuzi wa Mazingira" maana yake ni kama ilivyo tafsiriwa katika Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

"Udongo"maana yake ni kama ilivyo tafsiriwa katika Sheria ya Mazingira 2004.

"Vitu hatari" Maana yake ni kama ilivyo tafsiriwa katika Sheria ya Mazingira 2004.

## SEHEMU YA PILI
### MASHARTI YA UFUGAJI

Wajibu wa mfugaji

4. Kila Mfugaji chini ya Sheria Ndogo hizi:-

(a) atatakiwa kufuga idadi ya mifugo kama atakavyoelekezwa na Halmashauri.

(b) atatakiwa kufuga na kulisha mifugo yake katika maeneo ya malisho yaliyopangwa na Halmashauri.

(c) atatakiwa kupitisha mifugo yake katika njia zilizopangwa na kutengwa na Halmashauri.

(d) atatakiwa kuwa na kadi ya mifugo itakayo onyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo.

(e) atatakiwa kupeleka mifugo katika majosho kama atakavyo agizwa na Halmashauri.

(f) atatakiwa kuweka alama kwenye mifugo yake kama itakavyoelekezwa na Halmashauri.

Masharti kwa Mfugaji

5. Ni marufuku kwa mfugaji au mtu yeyote:-

(a) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani.

(b) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kupata kibali kutoka kwa Halmashauri.

(c) kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali cha Halmashauri.

(d) kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa na Halmashauri.

(e) kufuga mifugo mingi katika eneo dogo.

(f) kuchunga, kulisha au kunywesha maji mifugo katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shuhguli hiyo

Kudhibiti mifugo inayozurua hovyo

6.-(1) Halmashauri itakamata mfugo wowote utakao onekana unazurura hovyo au kulishwa katika maeneo yasiyoruhusiwa katika eneo la Halmashauri na kutozwa viwango vya faini kama ilivyoanishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Mfugo wowote utakao kamatwa utalipiwa faini kama itakavyo pangwa na Halmashauri.

(3) Endapo mwenye mfugo hatatokea ndani ya kipindi cha siku saba tangu kukamatwa kwa mifugo hiyo, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuuza kwa mnada mfugo huo baada ya kupata idhini ya Mahakama.

## SEHEMU YA TATU:
### KILIMO NA UHIFADHI WA ARDHI

Taratibu za Kilimo Sura ya 113 na 114

7.-(1) Mtu yeyote atakayetaka kuendesha shughuli za kilimo katika Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za kilimo kwa kuzingatia Kalenda ya Kilimo ya Halmashauri na kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi.

(2) Itakuwa halali kwa Halmashauri kuingia katika shamba lolote kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Kibali cha kuchoma moto

8.-(1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kusafisha shamba kwa kuchoma moto isipokuwa kwa kibali cha Halmashauri.

(2) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analotaka kuchoma moto.

(3) Muda unaoruhusiwa kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo hizi ni kuanzia saa 12:00 alfajiri hadi saa 4:00 asubuhi.

Hifadhi wa Mazingira

9.-(1) Chini ya Sheria Ndogo hizi Halmashauri itaweka utaratibu itakaoona unafaa kuhifadhi mazingira yaliyo chini ya mamlaka yake.

(2) Halmashauri itatenga maeneo maalum kwa ajili ya makazi, viwanda, biashara, kilimo, na malisho chini ya mpango wa matumizi bora ya ardhi.

(3) Halmashauri itakuwa na wajibu wakupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya kitaalam kutoka kwa Afisa Misitu.

Namna ya kuhifadhi mazingira

10.-(1) Halmashauri itatenga njia maalum ya kupitisha mifugo kwenda na kurudi kwenye malisho maalum au minadani.

(2) Halmashauri itafanya sensa ya mifugo na kutoa kadi ya mifugo na elimu ya ufugaji bora kwa jamii.

(3)Halmashauri haitaidhinisha kibali cha ujenzi wa jengo au nyumba ya aina yeyote ile katika eneo la hifadhi ya mazingira.

(4) Masharti ya kifungu kidogo cha (3) hayataathiri ujenzi wa jengo au nyumba endapo ujenzi huo unalenga kutekelezwa kwa shughuli za uhifadhi wa mazingira, au ni kwa ajili ya mradi wa uhifadhi wa mazingira.

(5)Halmashauri, mtu yeyote au kikundi cha watu kilichoidhinishwa na Halmashauri kitakamata mifugo au mfugo utakaoonekana unazurura hovyo katika eneo la Halmashauri ambapo haijaruhusiwa kuchungia mifugo na kuwekwa katika eneo maalum litakaloamriwa na Halmashauri.

(6) Mmiliki wa Mfugo au mifugo iliyokamatwa chini ya kifungu kidogo cha (5) cha Sheria Ndogo hizi atatozwa faini kwa kiwango kilichoidhinishwa na Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi.

(7) Endapo mmiliki wa mifugo au mfugo uliokamatwa atashindwa, atakaidi au atadharau ulipaji wa faini iliyoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hizi ndani ya siku saba tangu tarehe na siku ya kupewa taarifa ya ukamataji huo, Halmashauri itauza mfugo au mifugo na kuweka fedha katika akaunti ya Amana ya Halamshauri.

(8) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (7), Halmashauri itakokotoa faini inayostahili kulipwa pamoja na gharama nyinginezo zitokanazo na ukamataji na uhifadhi wa mifugo hiyo na endapo kuna kiasi kimesalia kitarejeshwa kwa mmiliki wa mifugo au mfugo uliouzwa.

(9) Endapo mifugo au mfugo uliokamatwa utakufa, Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote aliyoipata mmiliki isipokua kama kifo cha mifugo hiyo kimesababishwa na uzembe wa Halmashauri au watumishi wake.

11. Mtu yeyote hataruhusiwa kujenga nyumba au jengo lolote katika eneo ambalo Halmashauri imetangaza kuwa eneo la Hifadhi. Ujenzi Holela

## SEHEMU YA NNE
### HIFADHI YA VYANZO VYA MAJI

12.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu ndani ya Halmashauri kupanda miti isiyonyonya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Misitu. Wajibu wa Kulinda Vyanzo vya Maji

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuishi, kulima, kukata miti, kuchunga mifugo au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote eneo lililotangazwa kuwa eneo la hifadhi au chanzo cha maji.

(3)Ni marufuku kwa mtu yeyote kumiliki eneo la chanzo cha maji kilichopo ndani ya Halmashauri.

13. Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa mtu yeyote kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito, mabwawa, ziwa, visima, mifereji, chemchem au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai. Uchafu wa vyanzo vya maji

## SEHEMU YA TANO
### UHIFADHI WA MISITU

14.-(1) Mtu yeyote hataruhusiwa kukata miti katika maeneo ya misitu iliyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Halmashauri. Kuchoma au kusababisha moto

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa kuchoma moto misitu kwa namna yoyote ile katika misitu iliyoko eneo la Halmashauri.

(3) Iwapo moto utatokea katika eneo la Halmashauri na ukaonekana kuwa na madhara kwa maisha, mali za watu na uharibifu wa mazingira katika eneo husika, kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa amri kwa wakazi wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo.

(4) Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto huo endapo atatakiwa kufanya hivyo, kama atashindwa kushiriki katika kuzima moto bila sababu ya msingi atakuwa ametenda kosa.

Ukataji miti

15.-(1) Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa mtu yeyote kuvuna miti pasipo kuwa na kibali cha uvunaji wa miti.

(2) Afisa Misitu atatakiwa kuhakiki kama miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.

(3) Watu wanao vuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa, watatakiwa kuwa na eneo maalum lililoidhinishwa na Afisa Misitu kwa ajili ya kuchomea mkaa huo.

(4) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalumu ambao ni rasilimali kwa Taifa.

Wajibu wa kupanda miti

16. Kila mkazi wa Halmashauri atawajibika kupanda na kutunza miti katika eneo lake kama atakavyoelekezwa na Halmashauri.

## SEHEMU YA SITA
### TAKA NGUMU NA LAINI

Utupaji wa taka ngumu na laini

17.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila Mtu ndani ya Halmashauri kuwa na shimo kwa ajili ya kutupa taka ngumu na laini na kusimamia kwa karibu usafi katika eneo lake.

(2) Mtu yeyote atakayetupa taka ngumu au laini, kujisaidia katika mito, ziwa, mabwawa au kwenye vyanzo vya maji vilivyoko katika Halmashauri atakuwa ametenda kosa.

Uendeshaji wa viwanda

18. Itakuwa ni marufuku kuendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao, kukamua maji ya matunda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yoyote inayozalisha uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengine katika maeneo ya makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za ujenzi.

Gharama za utupaji taka

19 Halmashauri itatoza gharama za utupaji wa taka katika jalala (dampo) kutoka kwa mawakala, wamiliki wa taasisi mbalimbali, viwanda na makampuni pamoja

na wazalishaji wengine wa taka kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

## SEHEMU YA SABA
### MAKOSA NA ADHABU

20. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo; Makosa

(a) ataingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali.

(b) atasafirisha mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali.

(c) atasafirisha mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa.

(d) atafuga mifugo zaidi ya idadi iliyoruhusiwa,

(e) atakiuka masharti ya kilimo, kuchimba mchanga, kokoto, madini katika maeneo yasiyoruhusiwa.

(f) atakiuka masharti ya kuhifadhi ardhi.

(g) ataharibu vyanzo vya maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji.

(h) atabainika kuwa ameweka sumu ya aina yoyote kwa namna yoyote ambayo inaathiri maisha ya binadamu na viumbe wengine.

(i) atachoma au kusababisha moto katika misitu

(j) atakataa au atashawishi watu wengine kukataa kushiriki katika kuzima moto(k) atavuna mazao ya misitu bila kibali

(l) atachoma mkaa na kukata kuni bila kibali,

(m) atatupa hovyo taka ngumu au laini katika maeneo yoyote yasiyoruhusiwa Adhabu

(n) atatiririsha maji machafu yanayoleta madhara kwa binadamu na viumbe vingine hai.

(o) ataendesha shughuli za kiwanda au viwanda vidogo, karakana, mashine za kusaga na kukoboa nafaka mashine za kuranda mbao katika makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za mipango miji.

21. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa kiasi kisichozidi Shilingi elfu laki tatu (Tshs 300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

JEDWALI LA KWANZA

Limetungwa chini ya kifungu cha 6(1)

Faini za Mifugo inayozurura

| | **Aina ya Mifugo** | **Kiasi cha faini** |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 20,000/= kwa kilang'ombe |
| 2. | Punda | 10,000/= kwa kila punda |
| 3. | Mbuzi | 10,000/= kwa kila mbuzi |
| 4. | Kondoo | 10,000/= kwa kila kondoo |
| 5. | Nguruwe | 12,000/= kwa kilanguruwe |
| 6. | Mnyama mwingine yeyote | 5,000/= kwa kilamnyama |
| 7. | Gharama za ulinzi kwa siku kwa mnyama yeyote | 10,000/= kwa kila mnyama |

JEDWALI LA PILI

Limetungwa chini ya kifungu cha 19

Ada ya uzoaji taka

| | **Aina ya Biashara/mchangiaji** | **Kiwango cha ada kwa mwezi (tshs)** |
|---|---|---|
| 1. | Mgahawa mdogo/kibanda cha kuuzia chai au chakula | 1,000/= |
| 2. | Kioski na Glosari | 3,000/= |
| 3 | Nyumba za kulala wageni | 5,000/= |
| 4. | Zahanati | 3,500/= |
| 5. | Kituo cha Afya | 5,500/= |
| 6. | Mashine ya mbao katika mtaa wa viwanda vya mbao au eneo lolote lile katika Halmashauri | 5,000/= |

TANGAZO LA SERIKALI NA 733 *(Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Fundi Seremala | 5,000/= |
| 8. | Fundi chuma | 5,000/= |
| 9. | Karakana au gereji za magari | 5,000/= |
| 10. | Karakana nyinginezo | 200/= |
| 11. | Kiwanda kikubwa | 3,000/= |
| 12. | Kiwanda cha kati | 2,000/= |
| 13. | Kiwanda kidogo | 1,000/= |
| 14. | Duka la jumla/Super markets au mini super market | 3,000/= |
| 15. | Duka la rejareja | 2,000/= |
| 16. | Shule ya msingi ya bweni (kwa shule za watu na taasisi binafsi) | 3,000/= |
| 17. | Shule ya Sekondari ya Bweni(watu binafsi) | 3,000/= |
| 18. | Kituo cha kulelea watoto/ watu wenye mahitaji maalum | Bure |
| 19. | Duka dogo la vyakula | 2,000/= |
| 20. | Duka kubwa la vyakula | 5,000/= |
| 21. | Baa(Bar) | 5,000/= |
| 22. | Kumbi za starehe/disko | 5,000/= |
| 23. | Klabu za usiku/Night clubs | 5,000/= |
| 24. | Duka la kuuza samaki au nyama (bucha ya samaki au nyama | 2,000/= |
| 25. | Kibanda au kituo cha nyama choma/ chips kinachojitegemea | 1,000/= |
| 26. | Duka la dawa(jumla) | 2,000/= |
| 27. | Duka la dawa(rejareja) | 1,000/= |
| 28. | Dobi | 100/= |
| 29. | Fundi cherehani | 1,000/= |
| 30. | Saluni ya wanaume na wanawake | 3,000/= |
| 31. | Kibanda au mwavuli wa kuuza vocha | 500/= |
| 32. | Kituo cha kuuzia nishati ya mafuta (Filling station) | 5,000/= |
| 33. | Hotel kubwa | 10,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 34. | Ghala(Godown) | 5,000/= |
| 35. | Kiwanda cha mashine ya kukoboa mchele/nafaka | 3,000/= |
| 36. | Taasisi | 2,000/= |
| 37. | Washona viatu | 500/= |
| 38. | Wauza viatu vya mitumba/dukani | 500/= |
| 39. | Wauza nguo za mitumba | 500/= |
| 40. | Toroli la bidhaa au matunda | 500/= |
| 41. | Stoo za mkaa | 2,000/= |
| 42. | Stoo za mbao | 2,000/= |
| 43. | Mama/Baba lishe | 1,000/= |
| 44. | Duka la kuuzia vipali vya magari | 2,000/= |
| 45. | Kila Kaya | 1,000/= |
| 46. | Gari la kushusha mizigo (kila linaposhusha mzigo siku hiyo) | 2,000/= |
| 47. | Stationaries na maduka ya kuuza vitabu | 1,000/= |
| 48. | Duka la dawa baridi za binadam, duka la dawa za mifugo au pembejeo za kilimo | 1,000/= |
| 49. | Hospital | 10,000/= |
| 50. | Vyombo vya usafiri | 2,000/= |
| 51. | Watu au maeneo mengine | 1,000/= |

Lakii ya Halmashauri ya |wilaya ya Nanyumbu iligongwa kwenye Kanuni za Kudumu kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwan uliofanyika tarehe 28 mwezi Aprili Mwaka 2018 na iligwangwa mbele ya:-

PONSIA KAZEE
*Kaimu Mkurugenzi*
*Mtendaji Halmashauri ya Wilaya Nanyumbu*

**L.S**

AHAMAD B. MCHOPA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya Nanyumbu*

NAKUBALI

Dodoma,
14th September, 2019

SELEMANI S. JAFO (MB)
*Waziri wa Nchi-OR Tamisemi*